

Serikali yatangaza vita wavuvi haramu

Na Mbaraka Kambona, MWANZA

wa
ne-
eln
yo,
ko-
he-
nd
ioi-
re-
ko-
no
liye
ote
usi-
mi-
iwa
mo
Sh.

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema serikali itawekeza nguvu kubwa kukomesha uvuvi haramu katika Ziwa Victoria baada ya hatua kadhaa zilizo-chukuliwa awali ikiwamo kuwashirikisha wavuvi wa Kanda ya Ziwa kutokuzaa matunda.

Ndaki alitoa kauli hiyo alipokuwa akiongea na wadau wa sekta ya uvuvi katika kikao cha kujadili changamoto wanazokabiliana nazo wanaofanya shughuli zao katika Ziwa Victoria kilichofanyika mkoani Mwanza Mei 16, 2022.

Alisema mwaka jana serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya uvuvi waliandaa mpango shirikishi ambao ulianisha kila mdau na jukumu lake katika ulinzi wa rasilimali za uvuvi katika Ziwa Victoria, lakini matokeo yake wadau hao hawakujali na sasa uvuvi haramu umeongezeka maradufu.

"Uvuvi haramu sasa hivi ni mkubwa kwenye ukanda wetu wa Ziwa Victoria na sisi wizara tumepewa jukumu la kusimamia rasilimali hizi, Rais atatushangaa sana kuona wizara iliyopewa dhamana ya kuhakikisha rasilimali hizi zinalindwa, hazilindwi, sasa wakati tunatafuta mbinu endelevu ya kulinda rasilimali hizi, kuanzia sasa kwenda mbele tutatumia nguvu kuzuia uvuvi haramu," alisema.

Kadhalika alisema kuwa serikali haitavumilia watu wachache wenye kutaka kujinufaisha wao binafsi huku akiongeza kuwa watawashughulikia wote wanaojihusisha na uvuvi haramu kuanzia wavuvi, wasambazaji wa nyavu zisizo halali, na watakamata vyombo vyote vitakavyotumika kubebea au kuhifadhi mazao yaliyovuliwa kwa njia ya haramu katika mikoa yote inayozunguka ukanda wa ziwa.

Aidha, Waziri Ndaki aliwaeleza wadau wa uvuvi kuwa serikali imepokea changamoto zao na watazifanyika kazi, lakini nguvu kubwa kwa sasa itawekwa katika kupambana na uvuvi haramu kwa sababu kama rasilimali za uvuvi zikitoweka hizo changamoto nyingine kama za tozo na utafutaji wa masoko hazitakuwa na maana yoyote.

Naye Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anayeshughulikia sekta ya uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, alisema kuwa serikali imesikiliza kilio cha wavuvi kuhusu tozo na imezishughulikia kwa kiasi kikubwa na hivi karibuni michakato ikikamilika serikali itatoa maelekezo ambayo anaamini yatakuwa na nafuu kubwa kwa wavuvi.

ya Kiingereza